KENYA DAIRY BOARD

*"Quality milk for health and wealth"*

# MKATABA WA KUMHUDUMIA MWANANCHI

## KUANZISHWA

Bodi ya Maziwa ya Kenya, ni shirika lililoanzishwa katika mwaka 1958 kupitia kanuni ya Bunge kuhusu shughuli za Kiwanda cha Sekta ya Maziwa, kwa mujibu wa ibara ya 336 ya Sheria za Kenya.

## RUWAZA

Kuwa wakala wa Ulimwengu wa udhibiti wa Sekta ya Ubora wa Maziwa.

## WITO

Kudhibiti (kurekebisha) na kusimamia ubora uliopo pamoja na sekta endelevu ya maziwa.

## UTANGULIZI

**Mkataba wa kumhudumia mwananchi wa Bodi ya Maziwa ya Kenya unawakilisha kuwajibika kwetu katika kutoa huduma za hali ya juu kwa wadau wote. Sisi katika Bodi ya Maziwa ya Kenya, tunajitahidi kufikia na kupita matarajio ya wateja wetu kulingana na ahadi tulizoweka kwa Sekta ya Maziwa.**

| HUDUMA ZINAZOTOLEWA | MAHITAJI | MALIPO (KSH) | MUDA WA KUHUDUMIWA |
|---|---|---|---|
| Kushughulikia maswali ya wateja / kuomba kufahamishwa. | • Ushirikiano na maelezo wazi. | Bila malipo<br>Bila malipo<br>Bila malipo<br>Bila malipo<br>Bila malipo | • Kumhudumia mtu katika dakika tano (5) punde tu anapowasili kwenye ofisi ya Bodi.<br>• Kuthibitisha kupokea au kukubali baruapepe ni katika siku mbili (2 )za kazi.<br>• Kupata majibu ya maulizo au habari zilizotayari au zinazopatikana kwa urahisi katika siku 2.<br>• Kutoa majibu katika wiki mbili (2) kuhusu masuala magumu (maswala tata)<br>• Wateja wanaotumia simu watapata nafasi mara tatu (3) ya milio au mikirizo ya simu. |
| Takwimu ya Sekta ya Maziwa | • Ushirikiano na maelezo wazi. | Bila malipo | • Katika siku tano (5) za kazi. |
| Maulizo kwenye vyombo vya habari. | • Ushirikiano na maelezo wazi. | Bila malipo | • Katika siku mbili (2) kuanzia siku ya kupokea maulizo. |
| Kutatua malalamiko | • Kuwasilisha malalamiko<br>au<br>Mapendekezo ya Tume ya Kuridhia Haki. | Bila malipo | Utatuzi katika siku mbili (2) za kazi ikiwa taarifa iko tayari au inapatikana.<br>Utatuzi katika wiki tatu (3) endapo uchunguzi na mashauriano yanahitajika. |
| Utoaji wa ununuzi wa ndani (LPOs) au Kandarasi | • Makadirio / kutoa zabuni | Bila malipo | • Katika siku saba (7) za kazi baada ya kutoa zabuni (tenda) |
| Malipo kwa wasambazaji (wagavi) wa bidhaa na huduma | • Kandarasi / ununuzi wa ndani<br>• Kuwasilisha nyaraka/ ankara<br>• Ripoti ya ukaguzi | Bila malipo | • Katika siku thelathini (30) baada ya kupokea nyaraka / ankara |
| | LICENSES | | |
| Idhini Za Leseni | • Andaa mahali pa biashara kufikia kiwango cha ukaguzi.<br>• Toa maombi ili mahali pakaguliwe na Wakaguzi wa Bodi ya Maziwa.<br>• Ukaguzi utafanywa baada ya kulipa ada ya ukaguzi.<br>• Baada ya ukaguzi kufaulu, mteja atatuma maombi ya kupewa leseni ya mahali pa biashara kwa ada au malipo.<br>• Leseni itatolewa.<br><br>*Shauriana na Bodi ya Maziwa Kenya ukitaka maelezo zaidi.* | • Ada ya maombi sh. 600.<br>• Ada ya mtengenezaji sh.25,000.<br>• Ada ya mtoaji wa mwanzo (msingi) sh. 1,200.<br>• Ada ya Mashine ndogo ya kutoa maziwa sh. 6,000.<br>• Ada ya vibanda vya viwanda vidogo vidogo sh 4,000.<br>• Ada ya maduka ya kuuzia maziwa sh.2500.<br>• Ada ya kuhifadhi maziwa ( Lita 5,000 kurudi chini ) sh 1,000.<br>• Ada ya kuhifadhi maziwa (Lita 5,000 kuenda juu ) sh.2,000. | |


Mkurugenzi Mkuu
BODI YA MAZIWA KENYA, JUMBA LA SOCIAL SECURITY (NSSF) JENGO A, Upande wa Mashariki, ghorofa ya 10. S.L.P. 30404 - 00100 NAIROBI. Simu (020) 3569377 / 341302
RUNUNU: 0722573432 / 0733521438. Baruapepe: info@kdb.co.ke. Wavuti: www.kdb.co.ke
AU
Katibu wa Tume / Afisa Mtendaji Mkuu.Tume ya Utawala wa Haki,
Ghorofa ya pili, Mnara wa Magharibi Mwisho, Mkabala wa Barabara ya Waiyaki,
Westlands . S.L.P. 20414 - 00200 NAIROBI.